JINA……………………………………………………………KIDATO………………NAMBARI…………

102/3
KISWAHILI
Karatasi ya 3
FASIHI
MUDA: SAA 2 ½

**MTIHANIWA 6**

# 2018

## KIDATO CHA TATU

**MAAGIZO**

a) Jibu maswali manne pekee
b) Swali la kwanza ni la lazima
c) Maswali megine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki
d) Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja
e) Mtahiniwa ahakikishe kwamba kurasa zote za maswali zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**SEHEMU A**

1. **USHAIRI (LAZIMA)**

**Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.**

**WAPENDA MTU KWA KITU**

Shairi nakuleteya, tafadhali mwana twaa
Hikwita hunikimbiya, na kunitiya tamaa
Kumbe mebadiliniya, hata washenzi watwaa
Una mahaba tamaa, wapenda mtu kwa kitu.

Nilidhani u libasi, njema ya mtu kuvaa
Hawa sina wasiwasi, popote ninapokaa
Kumbe u mtu rakhisi, atakaye hukutwaa
Una mahaba tamaa, wapenda mtu kwa kitu.

Usinionye miuja, miuja haitafaa
Kwamba huna nami haja, ukanambia si baa
Mtu hupenda kimoja, sende nami kwa hadaa
Una mahaba tamaa, wapenda mtu kwa kitu.

Umejifunza wekevu, kutaka kunihadaa
Na huno wako uovu, ni bure hautafaa
Mimi ni wana mtuvu, sitendwi hataataa
Una mahaba tamaa, wapenda mtu kwa kitu.

Kunena mengi nataka, lakini sina wasaa
Na hapa tulipofika, ni kheri hakuambaa
Maana u mtu nyoka, huna ahadi ua baa
Una mahaba tamaa, wapenda mtu kwa kitu.

Tamati sineni sana, muhibu toa tamaa
Ulotenda nishaona, wala hutanihadaa
Sasa kheri kuatana, kulla mtu akakaa
Una mahaba tamaa, wapenda mtu kwa kitu.
***(A. Nasir, Malenga wa mvita, uk 163)***

**Maswali**

a) Kwa kurejelea vina vya shairi, eleza bahari ya shairi hili. (alama 2)
b) Eleza maana ya `una mahaba tamaa, wapenda mtu kwa kitu` (alama 2)
c) Je, msemaji analalamika mambo gani katika shairi? Eleza. (alama 3)
d) Eleza tabia za mhusika anayezungumziwa katika shairi hili. (alama 3)

e) Taja na ufafanue tamathali mbili za usemi zilizotumika katika shairi hili. (alama 4)
f) Eleza dhamira ya mtunzi. (alama 2)

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

g) Maneno yafuatayo yameendelezwa kishairi. Yaandike kwa njia sanifu. (alama 4)

i. Hikwita________________
ii. Kulla___________________
iii. Miuja ________________
iv. Kuatana________________

**SEHEMU B: TAMTHILIA**

**KIGOGO: PAULINE KEA**

4. ``Tunajivunia kuwa na kampuni kubwa zaidi ya uzalishaji sumu ya nyoka barani.''

a) Eleza muktadha wa kauli hili. (alama 4)

b) Andika mbinu moja ya lugha iliyotumika katika kauli hii. (alama 2)

c) Kwa kutumia mifano mwafaka, onyesha kwa hoja **kumi na nne(14)** jinsi sumu ya nyoka ilivyoathiri eneo la Sagamoyo katika tamthilia ya kigogo. (alama 14)

5. Fafanua jinsi mwandishi wa tamthilia ya kigogo alivyofaulu kutumia mbinu zifuatazo za uandishi.

a) Jazanda (alama 10)

b) Majazi (alama 10)

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com

**SEHEMU C**
**HADITHI FUPI**
**Tumbo Lisiloshiba *na Hadithi Zingine* - (S.A MOHAMMED)**

2. Fafanua maudhui manne yanayojitokeza katika hadithi ya Tumbo Lisiloshiba. (**alama 20**)

**SEHEMU D: FASIHI SIMULIZI**

3.

a. Fafanua maana ya istilahi zifuatazo (al 5)
   i. Kisasili
   ii. Lakabu
   iii. Kitendawili
   iv. Ushairi simulizi
   v. Ngomezi

b.
   i. Taja vianzio viwili vya ngano (al 2)
   ii. Eleza majukumu matatu ya vianzio vya ngano (al 3)

c.

i. Eleza sifa mbili za mtambaji bora (al 2)

ii. Tambulisha nyiso (al 1)

iii. Jadili majukumu mawili ya nyiso katika jamii (al 2)

d. i. Eleza maana ya misimu (al 2)

ii. Fafanua sifa za misimu (al 3)

for free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com